| Jina la Kisayansi | Jina la Kiswahili | Jina la Kiengereza |
|---|---|---|
| *Thunnus albacares* | Jodari mapezi njano | Yellowfin tuna |
| *Katsuwonus pelamis* | Zanuba/Sehewa mraba | Skipjack |
| *Thunnus obesus* | Jodari macho makubwa | Bigeye tuna |
| *Thunnus alalunga* | Jodari msumari | Albacore tuna |
| *Thunnus tonggol* | Jodari mkia mrefu | Longtail tuna |
| *Euthynnus affinis* | Sehewa | Kawakawa |
| *Auxis thazard* | Sehewa damudamu | Frigate tuna |
| *Auxis rochei* | Sehewa risasi | Bullet tuna |
| *Scomberomorus commerson* | Nguru | Narrow barred Spanish Mackerel |
| *Scomberomorus guttatus* | Wahoo/Nguru mkondo | Indo-Pacific king mackerel |
| *Makaira nigricans* | Samusuli buluu | Blue Marlin |
| *Makaira indica* | Samusuli mweusi | Black Marlin |
| *Tetrapturus audax* | Samusuli mistari | Striped Marlin |
| *Istiophorus platypterus* | Mbasi kuti/Nduwaro kuti | Indo-Pacific Sailfish |
| *Xiphias gladius* | Nduwaro/Mbasi | Swordfish |



*Jodari msumari*




***Kimetayarishwa na***

*Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu*
*S. L. P 56, Zanzibar - Tanzania*
*Namba ya simu: +255 779888241/779888215*
*Barua pepe: info@dsfa.go.tz*
*Tovuti: www.dsfa.go.tz*

***Kimefadhiliwa na***

*Southwest Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Program (SWIOFish).*

THE WORLD BANK

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

DSFA TANZANIA

# MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU




# MAENEO YA UWEKEZAJI KATIKA UVUVI WA BAHARI KUU TANZANIA

## 1. Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Tanzania

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina eneo la Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone - EEZ*) maarufu kama Bahari Kuu, lina ukubwa wa kilomita za mraba 223,000. Eneo hili linaweza kuvuliwa na meli zaidi ya 90 kwa mwaka. Shughuli za uvuvi katika EEZ husimamiwa na kuratibiwa na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) chini ya Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 na Kanuni zake za mwaka 2021.

Ramani inayoonesha mgawanyiko wa Bahari (EEZ)




## 2. Fursa za uwekezaji

Fursa za uwekezaji katika Bahari Kuu ya Tanzania ni pamoja na:-

a) Ujenzi wa miundombinu kuwezesha meli za uvuvi kufunga gati, kushusha au kuhaulisha samaki kutoka meli moja kwenda nyingine, kusafirishwa nje ya nchi au kuhifadhiwa na kuchakatwa viwandani;

b) Kufanya shughuli za uvuvi wa samaki aina ya Jodari na jamii zake;

c) Kuwekeza katika meli za kutoa huduma muhimu kwenye meli za uvuvi: maji, chakula, mafuta, vifaa na zana ya uvuvi ikiwa ni pamoja na vifaa vya kuvutia samaki (FADs);

d) Viwanda vya kuchakata na kusindika samaki na mazao mengine ya uvuvi ili kuongeza thamani kwenye mnyororo wa thamani wa samaki;

e) Ujenzi wa mitambo ya kutengeneza barafu na kuhifadhi samaki na mazao yake;

f) Kusafirisha samaki na bidhaa zake nje ya nchi;

g) Kutoa huduma na vifaa muhimu vinavyohitajika katika shughuli za uvuvi;

h) Ujenzi wa chelezo na karakana ya kutengeza na kukarabati meli za uvuvi na vifaa/zana za uvuvi, mfano nyavu za uvuvi, FADs; na

i) Ufugaji wa samaki kwa ajili ya chambo (baits) katika uvuvi wa mishipi (longliners).

## 3. Vivutio katika uwekezaji wa Bahari Kuu

Kwa mujibu wa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 na Kanuni zake za mwaka 2021, vivutio vinavyoweza kutolewa ni pamoja na:-

a) Punguzo la ada ya leseni za uvuvi kwa wazawa (asilimia 84 kwa uvuvi wa mishipi na 70 kwa uvuvi wa kuzungusha n.k.);

b) Uwezo wa kuingia ubia na makampuni ya nje na kupata punguzo la ada na tozo mbalimbali;

c) Uwezo wa kuomba lesseni ya uvuvi bila kupitia kwa wakala;

d) Misamehe mengine ya kodi, tozo, vifaa na mikopo yenye masharti nafuu itakayotangazwa na Serikali.

## 4. Vigezo na masharti ya vivutio

Mtu yeyote anayekusudia kuwekeza katika Bahari Kuu atapaswa kutimiza masharti na vigezo ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

a) Mpango yakinifu wa uwekezaji wa miaka mitatu;

b) Mpango wa biashara ambao pia utaainisha mapato ya mwaka;

c) Uwezo wa kusimamia na kuendesha biashara husika.

## 5. Aina za samaki wanaopatikana katika Bahari Kuu ya Tanzania

Tanzania imejaliwa kuwa na aina nyingi ya samaki wa biashara ikiwa ni pamoja na jamii 15 za Jodari na jamii zake, ambao hupatikana katika misimu miwili kwa mwaka (Mei hadi Septemba na Oktoba hadi Machi).